# MTIHANI WA KUTATHMINI WA MENTOR - 2020
## DARASA LA 8
## KISWAHILI (LUGHA)

**Muda:** Saa 1 dakika 40

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI**

1.Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu kina maswali 50.

2.Ukiisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha kwamba umeandika yafuatayo katika karatasi ya majibu.

**NAMBA YAKO YA MTIHANI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE YAKO**

5. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzoni mwa karatasi ya majibu.
6. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
7. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
8. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C. D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi.Chagua jibu hilo.
9. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

Katika kijitabu cha maswali:

**20.** Kanusha.

Kujali kwangu kumenisaidia

A. kutojali kwangu kutomenisaidia
B. kutojali kwangu kujanisaidia
C. kutojali kwangu hakujanisaidia
D. kujali kwangu kutomenisaidia

Jibu sahihi ni C

**Katika karatasi ya majibu:**

1. [A] [B] [C] [D] 10. [A] [B] [C] [D] 20. [A] [B] [C] [D] 30. [A] [B] [C] [D] 40. [A] [B] [C] [D]

katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 20, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

10. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
11. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Geuza Ukurasa**

© *Sanali Ventures Limited*

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo chini. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa kujaza kila pengo.***

Ni jukumu ______1______ kila mzazi kama mlezi___2______ wajibu wake ___3________ .______4_______ tunapoona baadhi yao ___5___watoto wao_____6_______ wenyewe. Kwa jumla jamii inafaa____7______ipasavyo. Hamna haja kufurahia unapomwona ___8____ wa jirani akipotea njia.

Walimu na wenye ____9____ ni_______10___ chema katika jamii. Wana uwezo wa kubadili mambo yanapozidi unga. Tuungane pamoja kwa kuwa_____10_______.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. wa | B. ya | C. la | D. za |
| **2.** | A. kutelekeza | B. kutekeleza | C. kuelekeza | D.kuteleza |
| **3.** | A.ipasvyo | B. inavyopaswa | C.itakavyopaswa | D.ilivyopaswa |
| **4.** | A. itasikitisha | B. ilisikitisha | C.husikitisha | D.inasikitisha |
| **5.** | A.wakiwapotosha | B.wakiwatosha | C.wakwaelekeza | D.wakiwatunza |
| **6.** | A.kwenyewe | B. vyenyewe | C.yenyewe | D. wenyewe |
| **7.** | A. kujumuika | B.kujulikana | C. kuwajibika | D.kutengana |
| **8.** | A. mzazi | B.daktari | C.mtoto | D. seremela |
| **9.** | A.hedhi | B.hadhi | C.hari | D.hamu |
| **10.** | A. kielekezi | B.kilelezo | C.vielelezi | D.kielelezo |

**11.** A. Mcheka kilema hafi hakijamfika
B. ukiona vyaelea jua vimeundwa
C. Haba haba hujaza kibaba
D. umoja ni nguvu utengano ni udhaifu

Waridi alifika darasani mapema siku hiyo, aliitoa shanta yake aliyokuwa____12_____ mgongoni. Baadaye alijiunga na wenzake kwa kuwa alipenda______13______ na kila mtu. Mwalimu aliingia na akaanza kufunza________14__, yaani maneno yanayotatanisha yanapotamkwa. Hicho kilikuwa kipindi ____15____ kujifunza msamiati.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **12.** | A. ameitwika | B. ameiangata | C. ameipakata | D. ameieleka |
| **13.** | A. kutengana | B.kutangamana | C.kutangana | D.kukaa |
| **14.** | A.visawe | B.vitawe | C. vitate | D.vitenzi |
| **15.** | A.la | B.vya | C. cha | D.za |

***Kuanzia swali la 16 hadi 30, jibu kila moja kulingana na maagizo uliyopewa.***

**16.** Chagua mapambo ambayo huvaliwa miguuni pekee.
- A. kipini,furungu
- B. Usinga,udodi
- C. Jebu,kikero
- D. Furungu,udodi

**17.** Kutokana na nomino safari tunapata nomino zifuatazo isipokuwa.
- A. Usafiri
- B. Msafiri
- C. Kusafiri
- D. Safiri

**18.** Tambua aina ya maneno yaliyopigwa mstari katika sentensi hii:

Natasha alirudisha karatasi <u>tatu</u> <u>afisini</u>.
- A. Kivumishi nomino
- B. Kivumishi kiunganishi
- C. Kielezi, kivumishi
- D. Kivumishi, kielezi

**19.** Chombo cha chuma kilichofungwa kamba cha kupimia usawa wa ukuta unaojengwa ni_______________?
- A. nyundo
- B. randa
- C. timazi
- D. patasi

**20.** Kitenzi, 'ogopa,' katika kauli ya kutendesha ni__________.
- A. ogopwa
- B. ogofya
- C. ogopeana
- D. ogopeshana

**21.** Mtu anayefanya kazi ya kufua vyuma huitwa.
- A. Mhunzi
- B. Mjume
- C. Mjumu
- D. Mnajimu

**22.** Badili sentensi ifuatayo katika wingi.

Chuma kilichovunjika kiliwekwa nyuma ya pazia.
- A. Vyuma vilivyovunjika viliwekwa nyuma ya mapazia.
- B. Chuma zilizovunjika ziliwekwa nyuma ya pazia.
- C. Vyuma vilivyovunjika viliwekwa nyuma ya pazia.
- D. Machuma yaliyovunjika yaliwekwa nyuma ya mapazia.

**23.** Ukigawanya thuluthi ya nyanya mara tatu sawa utapata?
- A. Khumusi
- B. Tusui
- C. Nusu
- D. Sudusi

**24.** Chagua sentensi iliyoakifishwa vizuri.
- A. Salale, motto amesahau njia ya kwao?
- B. Je? Unamfahamu Bwana. Musa.
- C. Tulinunua vifaa vifuatavyo: dawa, rangi, mswaki na kalamu.
- D. Huree? Wachezaji walishagilia!

**25.** Chagua sentensi iliyo na maelezi sahihi.
- A. Halati ni kaka wa mama.
- B. Mtoto wa kaka au dada ni mpwa.
- C. Ami ni jina wanaloitana kaka na dada.
- D. Wifi ni dada wa mama.

*© Sanali Ventures Limited*

26. Nomino 'ufa, utete, ukuti na ufa,' hupatikana katika ngeli ipi?

A. U-U

B. U-YA

C. U-ZI

D. U-I

27. Chagua tamathali ya usemi iliyotumika katika sentensi ifuatayo.

Siku hizi Juma amemea pembe hasikii mawaidha ya walimu

A. methali

B. nahau

C. tanakali ya sauti

D. Kinaya

28. Kanusha sentensi ifuatayo:

Simu iliyonunuliwa imeharibika.

A. Simu isiyonunuliwa haikuharibika.

B. Simu iliyonunuliwa haijaharibika.

C. Simu isiyonunuliwa haitaharibika.

D. Simu isingenunuliwa isingeharibika.

29. Mtu anayehamia katika nchi nyingine na kufanya makao huko huitwa____________.

A. mkimbizi

B. mtalii

C. mlowezi

D. msaliti

30. Geuza sentensi ifuatayo katika hali ya udogo.

<u>Mzee alipiga ngoma kwenye mji.</u>

A. Zee lilipiga goma kwenye jiji.

B. Vizee vilipiga vigoma kwenye vijiji

C. Kizee kilipiga kigoma kwenye kijiji.

D. Mzee alipiga kigoma kwenye jiji.

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40</u>***

Maliasili ni mali ambayo hutokana na maumbile katika mazingira. Kenya imejaliwa maliasili mengi ambayo tunategemea katika uchumi wetu. Tunajivunia mlima Kenya ambao ndio mlima wa pili kwa urefu barani Afrika. Isitoshe mlima huu pia huwa na theluji ambayo huajabisha.

Pia tunalo ziwa Viktoria ambalo ndilo ziwa kubwa zaidi barani Afrika.

Mbali na hayo, pia tunao wanyama pori. Wanyama hawa wamewekwa katika mbuga za wanyama kama vile,Mara,Amboseli na Tsavo.

Mbuga ya Mara huvutia watalii ambao huja kushuhudia mamia ya nyumbu wanapovuka mto Mara kuelekea Serengeti.

Tunayo mito katika kila pembe ya nchi. Jamii zinazoishi karibu na mito hufaidika kwa uvuvi na unyunyuzaji maji mimea yao. Isitoshe, maji kutoka mito hii huzalisha nguvu za umeme. <u>Hakuna bamvua isiyo na</u> <u>usubi</u>. Hasara na maafa makubwa hutokea hasa msimu wa masika mito inapovunja kingo zake.

Bahari ya Hindi pia huvutia watalii wengi wa nje na ndani. Watalii hawa hufika pwani kijivinjari na kujiburudisha,shughuli za uvuvi na biashara ya hoteli hunoga na wengi hupata <u>riziki</u>.

Misitu yetu nayo imesheheni miti ya kiasili na ya kupandwa. Miti hii huwa malighafi ya kutengenezea samani,mbao,makaa,karatasi,miongoni mwa vitu vingine. Wanyama,ndege na wadudu wengi hupata mkazi na lishe kutoka mitini. Licha ya hayo miti husafisha hewa na huvutia mvua ambayo hukuza mimea na wakenya hupata lishe.

Kwa kweli tusipotunza mali hayo ya asili tuliyotunikiwa na Mola tutakuja kujuta baadaye. Tuwajibike kwa kujivunia na kuhifadhi urembo wa taifa letu.

---

31. Kulingana na ufahamu,Mali ya asili ni:
    - A. Mali ya wazazi
    - B. Wanyama pori na Bahari Hindi
    - C. Mali yanayoleta watalii katika uchumi wetu.
    - D. Mali ambayo hutokana na maumbile katika mazingira

32. Kulingana na kifungu, kuwa watalii huja mara________?
    - A. Kuburudika
    - B. Kuogelea
    - C. Kushuhudia nyumbu wanapovuka mto Mara.
    - D. Kuchimba madini

33. Kwa mujibu wa kifungu:
    - A. Mlima Kenya ndio mrefu zaidi duniani.
    - B. Ziwa Viktoria ndilo ziwa la pili kubwa barani Afrika.
    - C. Mara, Aboseli na Tsavo ndizo mbuga pekee nchini.
    - D. Theluji kwenye kilele cha mlima Kenya huajabisha.

34. Faida za miti zilizotajwa katika ufahamu ni zifuatazo isipokuwa
    - A. Kuunda samani
    - B. Kuchoma makaa
    - C. Kunadhifisha hewa
    - D. Kuvutia mvua.

35. Neno masika lina maana gani kama lilivyotumiwa kwenye kifungu?
    - A. Msimu wa mvua nyingi
    - B. Msimu wa jua kali
    - C. Kipindi cha uangukaji ya majani ya mti huanguka
    - D. Hali ya nchi kuwa kavu

36. Kulingana na ufahamu watalii wanaozuru pwani:
    - A. Hutoka ughaibuni pekee
    - B. Hutoka ughaibuni na humu nchini
    - C. Hutoka humu nchini pekee
    - D. Hutoka ughaibuni wengi kama watokao Kenya

37. Watalii wanapofika pwani:
    - A. Watu hushereheka
    - B. Watu huteseka kwa kukosa kazi
    - C. Biashara ya hoteli hunoga
    - D. Watu wengi hukosa ajira.

38. Neno, 'riziki' lina maana gani kama lilivyotumiwa kwenye kifungu?
    - A. Kutokuwa na kazi
    - B. Kujikinga wakati wa mvua
    - C. Mnyama anaishi msituni
    - D. Mapato yatokanayo na kazi.

39. Chagua methali ilivyo na maana sawa na, 'hakuna bamvua isiyo na usubi,' kama ilivyotumiwa kwenye kifungu.
   A. Mwiba wa kujichoma huambiwi pole
   B. Mtaka cha mvunguni sharti ainame
   C. Hakuna mchele unaokosa ndume
   D. Mtaka yote hukosa yote

40. Chagua kichwa mwafaka cha kifungu hiki.
   A. Mazingira
   B. Watalii
   C. Wanyama pori
   D. Mali asili

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50***

Maimuna alisimama kwenye roshani huku akiwaza na kuwazua.Alikilaumu kifo kilichouchukua uhai wa mama yake Zainabu. Machozi yalimtiririkia hasa alipokumbuka mateso aliyoyapitia mkononi mwa jamaa zake. Kutilia msumari moto kwenye kidonda,mwajiri wake alimwona kama punda.

Alizama zii katika mawazo yaliyomzunguka kama pia. Ghafla alianguka kwenye karai lililojaa nguo na kupoteza fahamu. Mwajiri wake alimfokea kwa kuwa alikuwa anachezea karai na kupoteza wakati.

Maimuna aliyapitia mateso ya kupokea kichapo cha mara kwa mara na kunyimwa chakula na hata upendo. Alichukiwa na familia ya mwajiri wake kiasi cha kumtendea mabaya yote. Asiye na wake ana Mungu. Siku moja Maimuna alipata nafasi ya kutoka nje ya lango la mwajiri wake. Siku hiyo alijihisi kama mfungwa aliyenusurika kutoka gerezani. Alitembea pasi na kujua alikokuwa akielekea bora tu ameyaondokea masaibu yaliyomsibu na kumnyima raha nyakati zote.

Baada ya kutembea kwa masafa marefu, alichoka akaregea kama utumbo wa samaki. Alijitoma katika hoteli moja na kuagiza chakula bila kijua angelipa na nini au ni nani angemlipia. Alipomaliza kula mhudumu alimkazia macho Maimuna na kudai malipo. Hapo kizaazaa kikazuka kama mzuka.

Pembeni aliketi mwanaume wa makamo aliyesitisha ugomvi na kulipa ile bili yote. Kwa kuwa Maimuna alikuwa amebalehe alikubali ombi la mwanaume huyo na akaandamana naye hadi kwake. Baada ya kipindi cha miaka mitatu ya kuchumbiana walifunga pingu za maisha na wakaishi maisha ya kutamanika.

41. Chagua maan ya neno, 'roshani,' kama ilivyotumiwa katika kifungu
   A. Sehemu ya kufulia nguo
   B. Sehemu iliyojitokeza mbele ya nyumba hasa ghorofa
   C. Sehemu iliyotengenezwa kuanikia nguo
   D. Sehemu maalum katika bafu

42. Ni kwa nini Maimuna alitiririkwa na machozi
   A. Aliteswa na jamaa zake
   B. Mawazo ya kifo cha mama yake
   C. Alichapwa na mwajiri wake
   D. Kunyimwa chakula na mwajiri wake

43. Mateso aliyoyapitia Maimuna ni pamoja na;
   A. Kufiwa,kuchapwa na kukaziwa macho
   B. Kunyimwa chakula,kupokea kichapo na kuchukiwa
   C. Kutopendwa,kuozwa na kufanyishwa kazi
   D. Kuwa mfungwa,kutokula na kuchapwa

44. Chagua tamathali gani iliyotumika katika sentensi ifuatayo:

   Alichoka akaregea mithili ya utumbo wa samaki.

   A. Chuku
   B. Isitiara
   C. Nahau
   D. Tashbihi

45. Kwa mujibu wa kifungu, Mwanaume aliyeketi pembeni alikuwa mwenye?
   A. Mkali
   B. Ujasiri
   C. Mwerevu
   D. Ukaidi

46. Maimuna alikuwa amebalehe. Hii ina maana kuwa?
   A. alikuwa amekasirika
   B. alikuwa mnono
   C. alikuwa amekomaa
   D. alikuwa ameteseka

47. Chagua methali ambayo haiwezi kulinganishwa na Maisha ya maimuna.
   A. Baada ya dhiki ni faraja
   B. Subira huvuta heri
   C. Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani
   D. Kalamu ya Mungu haikosi

48. Ukweli wa methali 'Asiye na wake ana Mungu,' ulidhihirika wakati?
   A. Maimuna alipokula chakula katika hoteli
   B. Maimuna alipotoroka na kwenda zake
   C. Maimuna alipolipiwa chakula
   D. Maisha ya Maimuna yalipobadilika na kuwa mazuri

49. Chagua kauli isiyokuwa sahihi kulingana na kifungu.
   A. Maimuna hakuwa na mtu wa kutegemea kama mzazi
   B. Hatimaye maisha ya Maimuna yalichukua mkondo mpya
   C. Uamuzi wa Maimuna ulimletea maafa zaidi
   D. Uvumilivu wa Maimuna ulizaa matunda

50. Kichwa mwafaka zaidi cha taarifa uliyoisoma ni kipi?
   A. Haki za watoto
   B. Masaibu ya Zainabu
   C. Mwajiri katili
   D. Mawimbi ya maisha ya Maimuna.